**POTENT ACADEMY REVISION SERIES**
**SHUGHULI ZA KISWAHILI**
**GRADE 9 | MODEL 03**

**Jina________________________________________________ Tarehe ____________________**

*Jibu maswali yote kwa nafasi uliyopewa:*

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 7. Kwa kila nafasi, chagua jibu sahihi kati ya uliyopewa.**

Safari yetu ______ 1 ______ kijijini ilikuwa ______ 2 ______ sana. Tulianza ______ 3 ______ mapema asubuhi na kufika ______ 4 ______ alasiri. Njiani, tulipitia ______ 5 ______ misitu minene na mito mikubwa. Hali ya hewa ______ 6 ______ nzuri sana, na tulifurahia ______ 7 ______ hatua ya safari.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kutoka | B. kuelekea | C. ndani | D. nje ya |
| 2. | A. fupi | B. ndefu | C. rahisi | D. ngumu |
| 3. | A. kupanda | B. kuondoka | C. kutembea | D. kukimbia |
| 4. | A. asubuhi | B. usiku | C. jioni | D. adhuhuri |
| 5. | A. baadhi ya | B. nyingi | C. chache | D. zote |
| 6. | A. ilikuwa | B. ingekuwa | C. haikuwa | D. itakuwa |
| 7. | A. kila | B. zote | C. moja | D. chache |

**Kutoka swali la 8 hadi la 15, jibu maswali kulingana na maagizo.**

8. **Jaza nafasi kwa kutumia vihusishi sahihi.**

   a. Mti mrefu upo ______ darasa letu.

   b. Matendo alisimama ______ wazazi wake akipokea tuzo.

9. **Ripoti kauli zifuatazo kwa usahihi.**

*Download more Revision papers from www.potentacademy.com/resources*
Join our WhatsApp Revision group | Contact 07 01 23 83 83

a. "Njooni haraka twende sokoni," mama akawaambia wanawe.

---

---

c. "Leo sitakula chakula chochote," dada alisema.

---

---

10. **Badili sentensi ulizopewa katika kauli za mabanoni.**

a. Mwalimu amemsamehe mwanafunzi. (kutendwa)

---

---

b. Paulo anampenda mjomba wake. Mjomba wa Paulo anampenda Paulo. (kutendana)

---

---

11. **Jaza jedwali lifuatalo kwa usahihi.**

| **Nomino** | **Ukubwa** | **Udogo** |
|---|---|---|
| Jicho | i.____________________ | ii.____________________ |
| Ndama | i.____________________ | ii.____________________ |

12. **Andika sentensi hizi upya kwa kutumia amba-**

a. Wanafunzi walioonana walisalimiana.

---

b. Walio na vitabu vya hadithi waanze kuvisoma.

*Download more Revision papers from www.potentacademy.com/resources*
Join our WhatsApp Revision group | Contact 07 01 23 83 83

13. **Kanusha kauli zifuatazo kwa ustadi.**

a. Ukila kwa pupa utapaliwa.

b. Ungalinisaidia ningalikushukuru.

14. **Taja nomino moja katika ngeli ya:**

a. U - ZI ______________________________

b. U-U ______________________________

15. **Andika sentensi zifuatazo katika wingi.**

a. Jana jua lilikuwa kali.

b. Darasani safi ni huku.

**<u>Kutoka swali la 16 hadi la 20, chagua jibu sahihi.</u>**

16. Ni sentensi gani iliyo katika hali ya kuendelea?

A. Mashabiki watakuwa wakishangilia wakati huo.

B. Nyumba nzuri zimejengwa huku mashambani.

C. Mashairi yakikaririwa kwa ustadi, huvutia wengi.

D. Nyota humetameta angani nyakati za usiku.

*Download more Revision papers from [www.potentacademy.com/resources](www.potentacademy.com/resources)*
Join our WhatsApp Revision group | Contact 07 01 23 83 83

17. Chagua jibu lenye kiambishi kinachofaa kujaza nafasi katika sentensi ifuatayo.

    Zulia ___ lifumwa vizuri.

    A. ki          B. zi          C. li          D. vi

18. Sentensi, **Kanga alimpikia nyanya yake uji**, inamaanisha **Kanga alipika uji ili nyanya yake anywe**.

    *Chagua jibu lenye maana nyingine ya sentensi hiyo.*

    A. Kanga alipika uji akiwa kwa nyanya yake.

    B. Kanga alipika uji kwa kuelekezwa na nyanya yake.

    C. Kanga alipika uji kwa niaba ya nyanya yake.

    D. Kanga alipika uji baada ya nyanya yake.

19. Ukanusho wa sentensi, **Amewekeza fedha zake kwenye mradi huo** ni:

    A. Hatawekeza fedha zake kwenye mradi huo.

    B. Hakuwekeza fedha zake kwenye mradi huo.

    C. Hangewekeza fedha zake kwenye mradi huo.

    D. Hajawekeza fedha zake kwenye mradi huo.

20. Chagua jibu lenye sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.

    A. Huree, tumeshinda mechi hiyo.

    B. Huree? Tumeshinda mechi hiyo.

    C. Huree: tumeshinda mechi hiyo.

    D. Huree! Tumeshinda mechi hiyo.

*Download more Revision papers from [www.potentacademy.com/resources](www.potentacademy.com/resources)*
Join our WhatsApp Revision group | Contact 07 01 23 83 83